4. A quorum at a meeting of the Board shall be two-thirds of the members.
- Resolution of the Board
5. A resolution at a meeting of the Board shall require the affirmative votes of one half of the members present except the Chairman, who shall have a casting vote.
- Minutes
6. The Board shall cause minutes of all proceedings of the Board to be entered in books kept for that purpose.

Passed in the National Assembly on the 31<sup>st</sup> March 2015.

THOMAS D. KASHILILAH  
*Clerk of the National Assembly*

SHERIA YA BARAZA LA VIJANA LA TAIFA YA MWAKA, 2015

MPANGILIO WA VIFUNGU

Kifungu Jina

SEHEMU YA KWANZA  
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Tafsiri.
3. Madhumuni ya Sheria.

SEHEMU YA PILI  
KUANZISHWA, MAMLAKA NA KAZI ZA BARAZA

4. Kuanzishwa kwa Baraza.
5. Muundo wa Baraza.
6. Kazi za Baraza.
7. Mamlaka ya Baraza.
8. Vyombo vya Baraza.
9. Baraza la Vijana la Mkoa.
10. Baraza la Vijana la Wilaya.
11. Baraza la Vijana la Kata
12. Baraza kugatua mamlaka.
13. Utangazaji wa maslahi.
14. Sekretarieti.
15. Uteuzi wa Katibu Mtendaji.
16. Majukumu ya Katibu.

SEHEMU YA TATU  
MIKUTANO YA BARAZA

17. Mkutano Mkuu.
18. Mkutano wa Vijana wa Mkoa.
19. Mkutano wa Vijana wa Wilaya.
20. Mkutano wa Vijana wa Wilaya

SEHEMU YA NNE  
UANZISHWAJI NA KAZI ZA BODI

21. Uanzishwaji wa Bodi.
22. Kazi za Bodi.
23. Uendeshaji wa shughuli za Bodi.


SEHEMU YA TANO  
MASHARTI YANAYOHUSU FEDHA

24. Fedha za Baraza.
25. Makadirio ya mwaka.
26. Hesabu na ukaguzi.

SEHEMU YA SITA  
MASHARTI YA JUMLA

27. Kanuni.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



NA.12 YA 2015

NAKUBALI,  
JAKAYA MRISHO KIKWETE

*Rais*

25 Aprili, 2015

**Sheria kwa ajili ya kuanzisha Baraza la Vijana Tanzania la Taifa, kuainisha masharti ya kisajili, mamlaka na majukumu yake; kwa ajili ya kuanzisha Mkutano Mkuu, Baraza la Vijana la Mkoa na Wilaya na masharti mengine yanayohusiana na hayo.**

[.....]

IMETUNGWA na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

SEHEMU YA KWANZA  
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

**1.-(1)** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Baraza la Vijana Tanzania ya mwaka 2015 na itaanza kutumika katika tarehe ambayo Waziri, kwa taarifa katika Gazeti, atateua.



Tafsiri

(2) Sheria hii itatumika Tanzania Bara.

2. Katika Sheria hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

“Baraza” maana yake ni Baraza la Vijana la Taifa lililoanzishwa chini ya kifungu cha 4;

“Bodi” maana yake ni Bodi ya Ushauri ya Baraza iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 21(1);

“Mkutano Mkuu” maana yake ni mkutano unaoanzishwa chini ya kifungu cha 17;

“mwaka wa fedha” maana yake ni kipindi cha miezi kumi na mbili kinachoishia tarehe thelathini mwezi wa Juni kila mwaka;

“Waziri” maana yake ni Waziri mwenye dhamana na masuala ya vijana kwa wakati huo;

“Sera ya Maendeleo ya Vijana ya Taifa” maana yake ni sera ya Taifa kuhusu vijana iliyotayarishwa na Wizara ambayo kwa wakati huu ina dhamana na masuala ya vijana; na

“kijana” kwa madhumuni ya Sheria hii, maana yake ni mtu mwenye umri wa miaka kati ya kumi na tano na thelathini na tano.

Madhumuni ya Sheria

3. Madhumuni ya Sheria hii yatakuwa ni-

(a) kuweka jukwaa la utekelezaji wa masuala ya vijana katika ngazi ya kata, Wilaya, Mkoa, Taifa na kimataifa;

(b) kuhamasisha kujitolea na kujitegemea miongoni mwa vijana;

(c) kuishauri Serikali kuhusu masuala yanayohusiana na maendeleo ya vijana;

(d) kuwatarisha vijana kubeba majukumu ili kuwawezesha kuwa na tabia njema, maadili na mienendo mema;

- (e) kutayarisha mazingira bora kwa ajili ya ushiriki wa vijana katika masuala yanayohusiana na utoaji wa maamuzi;
- (f) kujenga mtandao miongoni mwa vijana na wadau wengine;
- (g) kuendeleza umoja miongoni mwa vijana mbali na tofauti zao katika rangi, kabila, siasa, uchumi, dini, utamaduni, jinsia na maeneo wanayotoka.

**SEHEMU YA PILI**  
**KUANZISHWA, MAMLAKA NA KAZI ZA BARAZA**

Kuanzishwa  
kwa Baraza

**4.-(1)** Kunaanzishwa Baraza litakalojulikana kama Baraza la Vijana Tanzania.

(2) Baraza litakuwa ni shirika hodhi, kuendelea kurithiwa na kuwa na lakiri yake na kwa kutumia jina lake litakuwa na uwezo wa-

- (a) kushtaki na kushtakiwa;
- (b) kununua au vinginevyo, kutwaa na kumiliki na kutoza malipo kwa mali zinazohamishika na zisizohamishika;
- (c) kutoa mali zinazohamishika na zisizohamishika;
- (d) kukopa fedha; na
- (e) kutenda au kufanya vitu vingine au jambo lolote ambalo ni la lazima katika utekelezaji bora wa kazi zake chini ya Sheria hii ambalo linaweza kufanywa kisheria na shirika hodhi.

(3) Uanachama wa Baraza utakuwa wazi na wa hiari kwa:

- (a) vijana kutoka katika kata husika;
- (b) vyama vya vijana vilivyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria husika;

(c) vijana waliochaguliwa na Kamati ya Maendeleo ya Kata.

(4) Baraza litakuwa sio taasisi ya kisiasa na:

(a) halita fanya kazi zake;

(b) halita tekeleza mamlaka yake fanya tumia nguvu zake; au

(c) halita tekeleza majukumu yake,

kwa makusudi au kuwa jukwaa la utekelezaji wa itikadi za kisiasa za chama cha kisiasa.

(5) Masuala yanayohusiana na malipo ya wajumbe, muda wa kukaa madarakani, mikutano na masuala mengine ya taratibu za Baraza yatakuwa kama yalivyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria hii.

Muundo wa Baraza

5.-(1) Baraza litaundwa na-

(a) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti watakao chaguliwa na Mkutano Mkuu;

(b) mwakilishi mmoja kutoka katika Baraza la Vijana la Mkoa; na

(c) Katibu atakayeteuliwa chini ya kifungu cha 13 cha Sheria hii.

(2) Baraza linaweza kumualika mtu yeyote kuhudhuria kikao chake chochote isipokuwa mtu huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura.

(3) Mtu hatateuliwa kuwa Mwenyekiti isipokuwa kama-

(a) angalau ana shahada ya kwanza kutoka katika chuo kinachotambuliwa;

(b) ameonyesha uwezo wa uongozi na kuwaunganisha vijana pamoja;

(c) ana weledi katika au amechangia kikamilifu katika kuhamasisha ajenda ya maendeleo ya vijana;

- (d) ana uaminifu wa hali ya juu, maadili na ana muitikio katika mahitaji na matarajio ya vijana; na
- (e) ni kijana na raia wa Tanzania.
- (4) Uteuzi chini ya kifungu kidogo cha (1)(a) utataja jina na kutangazwa katika *Gazeti* la Serikali.

Kazi za  
Baraza

**6.-(1) Kazi za Baraza zitakuwa ni-**

- (a) kuhamasisha na kuendeleza ari ya kujenga umoja, utafa, kujitolea, kujitegemea na kujituma miongoni mwa vijana;
- (b) kuendeleza tafiti, kukusanya na kuchambua data katika masuala ya vijana;
- (c) kuendeleza mahusiano baina ya mashirika ya vijana na vyombo vingine ndani na nje ya nchi yenye madhumuni na maslahi yanayofanana;
- (d) kuendeleza na kuitangaza Sera ya Taifa ya Vijana na sera nyingine zinazohusu vijana;
- (e) kutambua shughuli na mipango inayohusu vijana, inayoendeshwa na makundi ya vijana, jumuiya zinazojihusisha na vijana, asasi zisizokuwa za serikali, makundi ya asasi za kiraia na mashirika mengine;
- (f) kuendeleza na kuhamisha usawa wa jinsia miongoni mwa vijana;
- (g) kuendeleza masuala yanayohusiana na watu wenye ulemavu miongoni mwa vijana;
- (h) kuishauri Serikali katika masuala yanayohusu Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana na ajenda ya vijana;

45 **Na.12** *Sheria ya Baraza la Vijana la Taifa* **2015**

- (i) kupitia Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana na sera nyingine zinazohusu vijana na kuishauri Serikali;
- (j) kuendeleza masuala yanayohusu vijana wenye ulemavu katika ngazi ya Taifa na Kimataifa;
- (k) kuchangisha fedha kwa kuzingatia Sheria za nchi kwa ajili ya program ya maendeleo ya vijana;
- (l) kuanzisha na kuzindua program husika ambazo zinaendeleza masuala ya kilimo, elimu, fedha, teknolojia, jamii na utamaduni;
- (m) kuhamasisha ushirikishwaji wa vijana katika vyombo vya maamuzi, bodi, wakala na tasisi na mashirika mengine ya umma; na
- (n) Kuhamasisha ujumuishaji wa ajenda ya vijana katika utayarishaji wa Sera za taasisi na mashirika ya umma.

Mamlaka ya Baraza

7.-(1) Baraza litakuwa na mamlaka kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake chini ya Sheria hii, na mahsus bila kuathiri ujumla wake, itakuwa na mamlaka ya-

- (a) kuingia kwenye mkataba;
- (b) kusimamia, kudhibiti, na kusimamia mali zake kwa utaratibu na malengo ya kuendeleza madhumuni ya kuanzishwa kwa Baraza;
- (c) kupokea zawadi yoyote, mikopo yenye masharti nafuu, misaada au mali ya wakfu inayotolewa kwa Baraza au fedha yoyote ambayo ni kwa ajili ya Baraza na kuzigawanya kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii;

- (d) kwa idhini ya Mkutano Mkuu, kuingia katika ushirikiano na vyombo au mashirika mengine ndani na nje ya Tanzania kama inafaa katika kuendeleza madhumuni ya kuanzishwa kwa Baraza;
- (e) kufungua akaunti ya benki au akaunti za benki kwa ajili ya fedha za Baraza ambamo kwayo fedha zote zinazopokelewa na Baraza zitawekwa na malipo yote ya Baraza yata lipwa.
- (f) kuunda kamati yoyote itakayosaidia utekelezaji wa kazi za Baraza.
- (2) Endapo Baraza limepokea zawadi, mikopo yenye masharti nafuu au misaada, itamfahamisha Waziri kuhusu upokeaji huo.
- (3) Baraza linaweza, kimaandishi, kumruhusu mjumbe au mfanyakazi kutumia kwa niaba yake, baadhi ya mamlaka yake kama itakavyoainishwa lakini katika utekelezaji wa mamlaka hayo na kiwango kilichowekwa na Baraza, itatolewa taarifa ndani ya muda uliowekwa katika mkutano wa Baraza.

Vyombo vya Baraza

**8. Muundo wa Baraza utajumuisha:**

- (a) Baraza la Vijana Tanzania;  
 (b) Baraza la Vijana la Mkoa;  
 (c) Baraza la Vijana la Wilaya;  
 (d) Baraza la Vijana la Kata; na  
 (e) Sekretarieti.

Baraza la Vijana la Mkoa

**9.-(1)** Kutakuwa na Baraza la Vijana la Mkoa katika kila Mkoa.

(2) Baraza la Vijana la Mkoa litaundwa na idadi ya wajumbe wasiyozidi hamsini.

47 **Na.12** *Sheria ya Baraza la Vijana la Taifa* **2015**

- (3) Kazi za Baraza la Vijana la Mkoa zitakuwa ni-
- (a) kuishauri Sekretarieti ya Tawala ya Mkoa katika masuala yanayohusu maendeleo ya vijana katika ngazi ya mkoa;
  - (b) kuchagua vijana wawili kwa ajili ya Mkutano Mkuu;
  - (c) kuchagua Mwenyekiti na Katibu wa Mkutano wa Baraza la Vijana la Mkoa;
  - (d) kufanya kazi nyingine yoyote kama itakavyoelekezwa na Baraza.

(4) Masuala yanayohusiana na utaratibu wa uteuzi wa wajumbe wa Baraza la Vijana la Mkoa, mikutano, akidi na masuala mengine ya utaratibu wa Baraza la Vijana la Mkoa utakuwa kama inavyoonyeshwa kwenye Jedwali la Pili la Sheria hii.

(5) Baraza la Vijana la Mkoa litasaidiwa na Sekretarieti ya Vijana ya Mkoa na litafanya kazi nyingine kama itakavyoelekezwa na Katibu Mtendaji.

Baraza la  
Vijana la  
Wilaya

**10.-(1)** Kunaanzishwa Baraza la Vijana la Wilaya katika kila wilaya.

(2) Baraza la Vijana la Wilaya litaundwa na wawakilishi wa vijana kutoka katika Kata kama itakavyo amuliwa na Baraza la Wilaya husika.

- (3) Kazi za Baraza la Vijana la Wilaya zitakuwa ni-
- (a) kuishauri Sekretarieti ya Tawala ya Wilaya katika masuala yanayohusu maendeleo ya vijana;
  - (b) kuchagua wajumbe wa Baraza la Vijana la Wilaya; na
  - (c) kumchagua Mwenyekiti na Katibu wa Mkutano wa Baraza la Vijana la Wilaya;
  - (d) kufanya kazi nyingine yoyote kama itakavyoelekezwa na Baraza au Baraza la Taifa la Mkoa.

**Na.12** *Sheria ya Baraza la Vijana la Taifa* **2015** **48**

(4) Masuala yanayohusiana na utaratibu wa uteuzi wa wajumbe wa Baraza la Vijana la Wilaya, mikutano, akidi na masuala mengine ya utaratibu wa Baraza la Vijana la Wilaya yatakuwa kama inavyoonyeshwa kwenye Jedwali la Tatu la Sheria hii.

(5) Baraza la Vijana la Wilaya litasaidiwa na Sekretarieti ya Vijana ya Wilaya na litafanya kazi nyingine kama itakavyoelekezwa na Katibu Mtendaji au Sekretarieti ya Vijana ya Mkoa.

Baraza la  
Vijana la  
Kata

**11.**(1) Kunaanzishwa Baraza la Vijana la Kata katika kila kata.

(2) Baraza la Vijana la Kata litaundwa na idadi ya wajumbe wasiozidi ishirini na tano kutoka kwenye vijiji/mtaa ndani ya Kata husika.

(3) Kazi za Baraza la Vijana la Wilaya la kata zitakuwa ni-

(a) kuishauri Sekretarieti ya Kata katika mambo yanayohusu maendeleo ya vijana katika ngazi ya Kata;

(b) kuchagua wajumbe wa Baraza la Vijana la Kata;

(c) kumchagua Mwenyekiti na Katibu wa Baraza la Vijana la Kata;

(d) kwa kusaidiana na Sekretarieti ya Kata na kufanya kazi nyingine yoyote kama litakavyoelekezwa na Katibu Mtendaji au Sekretarieti ya Wilaya; na

(e) kutekeleza kazi zote kama ilivyoelekezwa na Baraza la Vijana Tanzania kupitia Baraza la Vijana la Wilaya.

(4) Masuala yanayohusiana na utaratibu wa uteuzi wa wajumbe wa Baraza la Kata, mikutano, akidi na masuala mengine ya utaratibu wa Baraza la Vijana la Wilaya utakuwa kama inavyoonyeshwa kwenye Jedwali la Nne la Sheria hii.



Baraza  
kugatua  
mamlaka

**12.** Baraza linaweza, kimaandishi na kwa azimio la jumla au maalum, kugatua kwa Katibu Mtendaji au kwa afisa yeyote wa Baraza, utekelezaji wa mamlaka yake yoyote au kazi yake yoyote.

Utangazaji  
wa maslahi

**13.**-(1) Endapo mjumbe ana maslahi ya moja kwa moja au vinginevyo kwenye mkataba, mkataba unaopendekezwa au jambo jingine mbele ya Baraza na yupo kwenye Mkutano wa Baraza ambao suala la mkataba, mkataba unaopendekezwa au jambo jingine lolote linajadiliwa, mjumbe huyo baada ya kikao na mapema iwezekanavyo baada ya kuanza-

- (a) ataeleza ukweli na hatakuwa sehemu ya mjadala wa mkataba huo au masuala mengine yoyote;
- (b) hatapiga kura kwenye suala lolote linalohusiana na mkataba huo au jambo jingine lolote; na
- (c) hatahesabiwa katika akidi ya mkutano wakati wa mjadala huo.

(2) Endapo wengi wa wajumbe waliopo wanaamini kwamba uzoefu au utaalum wa mjumbe huyo ni muhimu katika mjadala wa mkutano huo, Baraza linaweza kumruhusu mjumbe huyo kushiriki katika mjadala huo kwa masharti ambayo yanaweza kuwekwa na Baraza, isipokuwa mjumbe huyo hatokuwa na haki ya kupiga kura katika jambo linalojadiliwa.

- (4) Katika mkutano wa Baraza, itakuwa ni lazima kwa mjumbe mwenye maslahi na jambo linalotaka kuamuliwa, kutangaza maslahi katika jambo hilo na baada ya hapo atakosa sifa za kushiriki katika mjadala wa jambo hilo.

(4) Utangazaji wa maslahi uliofanywa chini ya kifungu hiki utawekwa katika kumbukumbu za mkutano ambao utangazaji huo umefanyika.

50 **Na.12** *Sheria ya Baraza la Vijana la Taifa* **2015**

(5) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (4), mjumbe wa Baraza, Bodi au Kamati anatenda kosa na atawajibika kulipa faini ya shilingi milioni moja.

Sekretarieti

**14.**-(1) Kutakuwa na Sekretarieti ya Baraza.

(2) Sekretarieti itakuwa chini ya uongozi wa Katibu Mtendaji ambaye atakuwa Katibu wa Baraza.

(3) Katibu Mtendaji atasaidiwa na wafanyakazi wengine kama itakavyokuwa lazima kwa utekelezaji bora wa kazi za Baraza.

Uteuzi wa  
Katibu  
Mtendaji

**15.**-(1) Katibu Mtendaji atakuwa ni kijana atakayechaguliwa na Waziri kutoka kwenye orodha ya majina matatu yaliyopendekezwa na Baraza.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Katibu Mtendaji ambaye:

(a) angalau ana shahada ya kwanza kutoka katika chuo kinachotambuliwa;

(b) ameonesha uwezo wa uongozi na kuwaunganisha vijana pamoja;

(c) ana weledi katika au amechangia kikamilifu katika kuhamasisha ajenda ya maendeleo ya vijana;

(d) ana uaminifu wa hali ya juu, maadili na ana muitikio katika mahitaji na matarajio ya vijana;

(e) ni kijana na raia wa Tanzania.

(3) Katibu Mtendaji atakaa madarakani kwa kipindi cha miaka mitano au mpaka atakapofikia umri wa miaka thelathini na tano, au chochote kitakachotangulia mwanzo, kwa kuzingatia masharti ya kazi kama Baraza litakavyoamua.

(4) Katibu atakuwa, kupitia wadhifa wake, mjumbe wa Baraza na hatakuwa na haki ya kupiga kura katika mkutano wowote wa Baraza.

51	<b>Na.12</b>	<i>Sheria ya Baraza la Vijana la Taifa</i>	<b>2015</b>
Majukumu ya Katibu	<p><b>16.-(1)</b> Katibu, kwa maelekezo ya Baraza, atatekeleza majukumu yafuatayo:</p> <p>(a) kutekeleza maelekezo juu ya shughuli za Baraza;</p> <p>(b) kutekeleza na kusimamia madhumuni na kazi za Baraza.</p> <p>(2) Katibu-</p> <p>(a) atahakikisha kuwepo kwa ufanisi na nidhamu kwa wafanyakazi wote wa Baraza;</p> <p>(b) atasimamia bajeti ya Baraza ili kuhakikisha kuwa fedha za Baraza zinatumiwa ipasavyo na kuwekewa kumbukumbu za hesabu; na</p> <p>(c) atatekeleza majukumu mengine kama ambavyo, mara kwa mara, Baraza linaweza kumuelekeza.</p> <p>(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (2)(a), Baraza litakuwa ni mamlaka ya nidhamu kwa wajumbe na wafanyakazi wake.</p> <p>(4) Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (3), Katibu ataanzisha au kupeleka malalamiko yote kwenye kamati ya Baraza iliyoundwa mahsusi kwa ajili hiyo kabla ya kuwasilishwa kwenye Baraza kwa ajili ya maamuzi.</p> <p>(5) Waziri atatengeneza kanuni zinazoainisha masuala yanayohusiana na utaratibu wa kupokea na kushughulikia malalamiko na mambo mengine yanayohusiana na hayo.</p> <p>(6) Katibu atawasilisha, si zaidi ya miezi mitatu kabla ya kuanza kwa kila mwaka wa fedha, katika Baraza programu za utekelezaji wa Baraza mwaka huo wa fedha kwa ajili ya kupata ridhaa.</p> <p>(7) Katibu, kwa ridhaa ya Baraza, ataajiri idadi ya wafanyakazi kama atakavyoona inafaa kwa kazi za kila siku za Baraza.</p>		

**SEHEMU YA TATU  
MIKUTANO YA BARAZA**

Mkutano  
Mkuu

**17.**-(1) Mkutano Mkuu utakuwa ni chombo cha juu cha kutoa maamuzi cha Baraza.

(2) Kazi za Mkutano Mkuu zitakuwa-

- (a) kumchagua Mwenyekiti wa Baraza;
- (b) kupendekeza wajumbe wa Bodi ya Ushauri;
- (c) kuridhia mipango ya maendeleo, mikakati na programu za Baraza; na
- (d) kupokea, kutathamini na kuridhia utekelezaji wa mipango, mikakati na programu.

(3) Mkutano Mkuu utaundwa na:

- (a) Mwenyekiti wa Baraza;
- (b) Mwenyekiti na Katibu wa kila Mkoa wa Baraza la Vijana la Mkoa;
- (c) kila Mwenyekiti wa Wilaya wa Baraza la Vijana la Wilaya;
- (d) Katibu mtendaji; na
- (e) Wawakilishi watano mahsus kwa vijana wenye ulemavu,

Isipokuwa moja ya tatu ya watu waliochaguliwa watatoka katika jinsi moja wapo.

(5) Masuala yanayohusiana na mikutano, akidi na masuala mengine ya utaratibu wa Mkutano Mkuu utakuwa kama inavyoonyeshwa kwenye Jedwali la Nne la Sheria hii.

Mkutano wa  
Vijana wa  
Mkoa

**18.**-(1) Mkutano wa Vijana wa Mkoa utakuwa ni chombo cha juu katika masuala yanayohusiana na vijana katika ngazi ya Mkoa.

(2) Mkutano wa Vijana wa Mkoa utaundwa na:

- (a) Mwenyekiti wa Baraza la Vijana la Mkoa;

- (b) si zaidi ya wajumbe thelathini wa Baraza la Vijana la Mkoa; na
  - (c) wawakilishi wawili ambao ni wanachama wa chama cha vijana kutoka katika Wilaya mbali ya wajumbe wa Baraza la Vijana la Mkoa; na
  - (d) Katibu wa Baraza la Mkoa.
- (3) Kazi za Mkutano wa Vijana wa Mkoa zitakuwa ni:
- (a) kumchagua Mwenyekiti wa Baraza la Vijana la Mkoa;
  - (b) kutekeleza mipango ya maendeleo, mikakati, na programu za Baraza katika ngazi ya mkoa;
  - (c) kupendekeza ajenda za Mkutano Mkuu; na
  - (d) kufanya kazi nyingine yoyote kama itakavyoelekezwa na Mkutano Mkuu.
- (4) Masuala yanayohusu mikutano, akidi na masuala mengine ya taratibu za Mkutano wa Vijana wa Mkoa yatakuwa kwa kuweka marekebisho stahiki, kama inavyoonyeshwa katika Jedwali la Nne la Sheria hii.

Mkutano wa  
Vijana wa  
Wilaya

- 19.**-(1) Mkutano wa Vijana wa Wilaya utakuwa ni chombo cha juu katika masuala yote yanayohusiana na vijana katika ngazi ya Wilaya.
- (2) Mkutano wa Vijana wa Wilaya utaundwa na:
- (a) Mwenyekiti wa Baraza la Vijana la Wilaya;
  - (b) Katibu wa Baraza la Vijana la Wilaya; na
  - (c) Wajumbe wasiozidi thelathini wa Baraza la Vijana la Wilaya; na
  - (d) Wajumbe thelathini kutoka katika vyama vya vijana ndani ya Wilaya mbali na wajumbe wa Baraza la Wilaya la Vijana.
- (3) Kazi za Mkutano wa Vijana wa Wilaya zitakuwa ni:

- (a) kumchagua Mwenyekiti wa Baraza la Vijana la wilaya;
  - (b) kutekeleza mipango ya maendeleo, mikakati na programu za Baraza katika ngazi ya Wilaya;
  - (c) kupendekeza ajenda za Mkutano Mkuu kupitia Mkutano wa Vijana wa Mkoa; na
  - (d) kufanya kazi nyingine yoyote kama itakavyoelekezwa na Mkutano Mkuu.
- (4) Masuala yanayohusu Mikutano, akidi na masuala mengine ya taratibu za Mkutano wa Vijana wa Wilaya yatakuwa, kwa kuweka marekebisho stahiki, kama inavyoonyeshwa katika Jedwali la Tano la Sheria hii.

Mkutano wa  
Vijana wa  
Wilaya

20.-(1) Mkutano wa Vijana wa Kata utakuwa ni chombo cha juu katika masuala yanayohusiana na vijana katika ngazi ya Kata.

(2) Mkutano wa Vijana wa Kata utaundwa na:

- (a) Mwenyekiti wa Baraza la Vijana wa Kata;
- (b) Katibu wa Baraza la Vijana wa Kata;
- (c) wawakilishi watatu kutoka kwenye taasisi au vikundi vya vijana kwenye mtaa au kijiji husika ndani ya Kata;
- (d) wawakilishi wawili kutoka kila kijiji au mtaa.

(4) Kazi za Mkutano wa Vijana wa Kata zitakuwa ni:

- (a) kumchagua Mwenyekiti wa vijana wa Baraza la Vijana la Kata;
- (b) kutekeleza mipango ya maendeleo, mikakati na program za Baraza katika ngazi ya kata; na
- (c) kufanya kazi nyingine yoyote kama itakavyoelekezwa na Baraza la Vijana la Kata na Mkutano Mkuu.

**SEHEMU YA NNE  
UANZISHWAJI NA KAZI ZA BODI**

Uanzishwaji  
wa Bodi

**21.-**(1) Kunaanzishwa Bodi ya Ushauri ya Baraza.

(2) Bodi itaundwa na wafuatao-

(a) Mwenyekiti atakayeteuliwa na Rais;

(b) Mwenyekiti wa Baraza la Vijana Tanzania;

(c) Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Vijana;

(d) afisa sheria atakayemwakilisha Mwanasheria Mkuu; na

(e) vijana watano watakaochaguliwa na Baraza na kuridhiwa na Waziri.

(3) Mtu hatateuliwa kuwa Mwenyekiti isipokuwa kama mtu huyo-

(a) angalau ana shahada ya kwanza kutoka katika chuo kinachotambuliwa;

(b) ameonsha uwezo wa uongozi kwa vijana na kuwaunganisha vijana pamoja;

(c) ana weledi katika au amechangia kikamilifu katika kuhamasisha ajenda ya maendeleo ya vijana; na

(d) ana uaminifu wa hali ya juu, maadili na ana muitikio katika mahitaji na matarajio ya vijana.

Kazi za Bodi

**22.-**(1) Kazi kuu za Bodi zitakuwa ni kulishauri Baraza kwa ujumla katika utekelezaji wa mamlaka na kazi zake zilizoainishwa chini ya Sheria hii.

(2) Bodi itakuwa na kazi nyingine kama itakavyopewa au itakavyoelekezwa chini ya Sheria hii.

Uendeshaji  
wa shughuli  
za Bodi

**23.-**(1) Kazi na masuala ya Bodi yataendeshwa kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii.

(2) Wajumbe wa Bodi watalipwa ujira, ada, posho na malipo mengine kwa ajili ya matumizi kama itakavyoamuliwa na Waziri.

(3) Baraza linaweza kumwalika mtu yeyote kuhudhuria katika mikutano yake na kushiriki katika mijadala lakini mtu huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura katika maamuzi yoyote ya Bodi.

(4) Masuala yanayohusu kukaa madarakani, utaratibu wa uteuzi na masuala mengine ya utaratibu wa Bodi yatakuwa kama yalivyoonyeshwa katika Jedwali la Tano la Sheria hii.

SEHEMU YA TANO  
MASHARTI YANAYOHUSU FEDHA

Fedha za  
Baraza

**24.** Fedha na mali za Baraza zitajumuisha-

- (a) fedha zote kama zitakavyopangiwa matumizi na kwa madhumuni ya Baraza;
- (b) fedha zote au mali zinazoweza kuingia kwenye Baraza wakati ikitekeleza mamlaka yake au kutekeleza kazi zake chini ya Sheria hii au sheria nyingine yoyote;
- (c) michango kutoka mamlaka ya serikali za mitaa;
- (d) zawadi kama zinavyoweza kutolewa kwa Baraza; na
- (e) fedha zote kutoka chanzo chochote kilichotolewa, zilizochangwa au kukopeshwa kwa Baraza.

Makadirio  
ya mwaka

**25.**-(1) Angalau miezi mitatu kabla ya kuanza kwa kila mwaka wa fedha, Baraza litagiza kuandaliwa kwa makadirio ya mapato na matumizi yake kwa mwaka huo wa fedha na kuyawasilisha kwenye Bodi.



(2) Makadirio ya mwaka yataweka masharti ya makadirio ya matumizi ya Baraza kwa mwaka huo wa fedha, hususan-

- (a) malipo ya mshahara, posho na malipo mengine yanayohusu maafisa, wakala au wafanyakazi wa Sekretarieti;
- (b) malipo ya pensheni, kiinua mgongo na malipo mengine yanayohusu mafao ya uzeeni yanayolipwa kwa wafanyakazi wa Sekretarieti; na
- (c) kuhifadhi, kutengeneza na kubadilisha mitambo na mali zote zinazohamishika za Sekretarieti.

(3) Makadirio ya mwaka yataidhinishwa na Baraza kabla ya kuanza kwa mwaka wa fedha unaohusika, na mara itakapoidhinishwa, itawasilishwa kwa Waziri kwa ajili ya kuridhiwa na baada ya Waziri kuridhia, Baraza halitarekebisha makadirio ya mwaka bila ya idhini ya Waziri.

(4) Matumizi hayatofanywa kwa madhumuni ya Baraza isipokuwa kwa kuzingatia makadirio ya mwaka yaliyoidhinishwa chini ya kifungu kidogo (3) au kwa kuzingatia ridhaa ya Baraza iliyotolewa baada ya ridhaa ya maandishi ya Waziri.

Hesabu na ukaguzi

**26.-**(1) Baraza litahakikisha kutunzwa kwa vitabu vya mahesabu na kumbukumbu za mahesabu ya mapato, matumizi, mali na madeni ya Baraza.

(2) Baraza, ndani ya miezi mitatu kila baada ya mwisho wa mwaka wa fedha, litawasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hesabu za Baraza zinazohusu mwaka huo, pamoja na-

- (a) maelezo ya mapato na matumizi ya Baraza wakati wa mwaka huo wa fedha; na

58 **Na.12** *Sheria ya Baraza la Vijana la Taifa* **2015**

- (b) maelezo ya mali na madeni ya Baraza ya siku ya mwisho wa mwaka huo wa fedha.
- (3) Hesabu za Baraza zitakaguliwa na kutolewa taarifa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

SEHEMU YA SITA  
MASHARTI YA JUMLA

Kanuni

**27.**-(1) Waziri anaweza, kupitia mapendekezo ya Baraza, kutengeneza kanuni za jumla kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila ya kuathiri ujumla wa kifungu kidogo cha (1), Waziri atatengeneza kanuni zinazoainisha:

- (a) uundwaji wa kamati za Baraza;
- (b) majukumu ya mamlaka za serikali za mitaa kuhusiana na shughuli za Baraza la Mkoa, Baraza la Wilaya, Mkutano wa Mkoa na Mkutano wa Wilaya;
- (c) utaratibu wa uchaguzi wa wenyeviti, uteuzi wa Katibu na viongozi wengine katika ngazi ya mkoa na wilaya; na
- (d) masuala mengine yoyote yanayoweza kuainishwa katika Sheria hii.

**JEDWALI LA KWANZA**

(linatengenezwa chini ya kifungu cha 4(5))

**UJIRA WA WAJUMBE, MUDA WA KUKAA MADARAKANI, MIKUTANO NA MASUALA MENGINEYO YA UTARATIBU WA BARAZA**

- Ajira ya wajumbe wa Baraza
1. Wajumbe wa Baraza watalipwa posho na matumizi mengine kama itakavyoidhinishwa na Waziri.
- Muda wa kukaa madarakani
- 2.-(1) Mjumbe yeyote wa Baraza, mbali na mjumbe anayeingia kwa wadhifa wake, kwa kuzingatia masharti ya Jedwali hili, atakaa madarakani kwa muda usiozidi miaka mitatu, kwenye mashauri yatakayoanishwa kwenye hati ya uteuzi ya mjumbe huyo, lakini anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja.
- (2) Wajumbe wa Baraza watateuliwa kwa nyakati tofauti ili muda wao wakumaliza kipindi chao umalizike kwa nyakati tofauti.
- (3) Uteuzi wa Baraza utafanywa kwa kupitia Tangazo la Serikali.
- Uwazi wa ofisi
- 3.-(1) Mjumbe wa Baraza, mbali na mjumbe anayeingia kwa wadhifa wake, ataweza-
- (a) katika wakati wowote kuacha kazi katika ofisi kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa Waziri;
- (b) kuondolewa ofisi na Waziri kama mjumbe, iwapo-
- (i) hajahudhuria vikao vitatu mfululizo vya Baraza bila kupewa ruhusa na Mwenyekiti;
- (ii) amepatikana na hatia ya kosa la jinai au amehukumiwa kifungo;
- (iii) ameshindwa kutekeleza majukumu yake kutokana na magonjwa ya kiakili na kimwili kwa muda mrefu au hawezi kutekeleza majukumu yake kama mjumbe wa Baraza; au
- (iv) ameshindwa kufuata masharti ya Sheria hii.

60 **Na.12** *Sheria ya Baraza la Vijana la Taifa* **2015**Mikutano ya  
Baraza

4.-(1) Baraza litakutana mara moja kwa mwaka.

(2) Bila kujali masharti ya aya ndogo (1), Mwenyekiti au wajumbe watatu wengine wa Baraza wanaweza kuitisha mkutano maalum muda wowote pale inapohitajika kwa ajili ya shughuli za Baraza, kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa wajumbe katika siku zisizopungua saba.

(3) Wajumbe wa Baraza katika kikao cha kwanza cha Baraza, watachagua kutoka miongoni mwao Makamu Mwenyekiti.

(4) Isipokuwa robo tatu ya wajumbe wote wa Baraza wanakubali vinginevyo, angalau siku kumi na nne watatoa taarifa ya kila mkutano wa Baraza na kupewa kila mjumbe wa Baraza.

(5) Akidi ya uendeshaji wa shughuli za Baraza itakuwa ni mbili ya tatu ya wajumbe, bila ya Katibu.

(6) Mwenyekiti ataongoza kila kikao cha Baraza ambacho yupo, lakini asipokuwepo, Makamu Mwenyekiti ataongoza, na asipokuwepo, wajumbe waliopo watachagua mmoja kutoka miongoni mwao ambaye kwa ajili ya mkutano huo na shughuli inayofanywa hapo atakuwa na mamlaka yote ya Mwenyekiti.

(7) Isipokuwa kama maamuzi ya pamoja hayatafikiwa, maamuzi yoyote mbele ya Baraza yatakuwa ya wajumbe wengi waliopo na kupiga kura, na pale kura zitakapolingana, Mwenyekiti au mtu anayeongoza kikao hicho atakuwa na kura ya turufu.

(8) Kwa kuzingatia aya ndogo (5), taratibu za uendeshaji wa vikao vya Baraza havitokuwa batili kwa sababu tu ya kuwepo kwa nafasi wazi ya mjumbe katika kikao hicho.

(9) Azimio la maandishi au maazimio yaliyo yenye nyaraka mbalimbali zinazofanana, kila moja likiwa limetiwa sainsi na wajumbe wa Baraza, litakuwa halali na litatumika kama vile limepitishwa na kikao kilichoitishwa na kupitishwa kihalali.

(10) Kwa kuzingatia masharti ya Jedwali hili, Baraza linaweza kuamua utaratibu wake na utaratibu wa kamati yoyote ya Baraza na kuhudhuria kwa mtu yeyote katika mikutano na linaweza kutengeneza kanuni pamoja na mambo mengine kuhusu-

- (a) mwenendo na usimamizi wa masuala ya Baraza;
- (b) namna ya malipo yote ikijumuisha, hundi, hati fungani na hati nyingine za malipo na stakabadhi zote za fedha zilizolipwa kwenye Baraza, zitasainiwa, kutolewa, kukubaliwa, kupitishwa au vinginevyo kutekelezwa; na
- (c) taratibu za mikutano na shughuli nyingine za Baraza.

Kumbukumbu **5.** Baraza litasaidia kutayarishwa kwa kumbukumbu za maazimio yote na taarifa za mienendo ya mikutano ya Baraza kuwekwa katika vitabu maalum kwa ajili hiyo.

Lakiri ya Baraza **6.**-(1) Lakiri ya Baraza utahifadhiwa na Katibu au na mtu mwingine kama ambavyo Baraza litakavyoamuru, na hautatumika ila kwa amri ya Baraza.

(2) Lakiri ya Baraza, utakapopigwa katika nyaraka na kuthibitishwa, utakubalika na kutambulika kisheria na isipokuwa vinginevyo ikithibitishwa, amri yoyote au ridhaa ya Baraza chini ya kifungu hiki itachukuliwa kuwa imetolewa hivyo.

(3) Lakiri ya Baraza utathibitishwa kwa kutiwa saini ya Katibu wa Baraza.

**JEDWALI LA PILI**

*(Linatengenezwa chini ya kifungu cha 9(4))*

**UTEUZI, MUDA WA KUKAA MADARAKANI, MIKUTANO NA MASUALA  
MENGINEYO YA  
UTARATIBU WA BARAZA LA MKOA**

Muundo wa Baraza la Vijana la Mkoa **1.** Baraza la Vijana la Mkoa litaundwa na:  
(a) Mwenyekiti;  
(b) Wajumbe wote wa Kamati ya vijana mkoa; na  
(c) vijana thelathini watakaowakilisha Baraza la vijana la wilaya.

Jukumu la mamlaka ya serikali za mitaa **2.** Mamlaka ya Serikali za mtaa katika eneo la Baraza la vijana la mkoa litakuwa na jukumu la uangalizi wa kazi na muundo wa Baraza la vijana Mkoa.

- Uundwaji wa Kamati ya Baraza la Vijana la Mkoa
- 3.-**(1) Baraza la Vijana la Mkoa litaunda Kamati itakayoitwa Kamati ya Vijana Mkoa.
- (2) Kamati ya Vijana ya Mkoa itakuwa chombo cha Baraza la Vijana Mkoa.
- Muundo wa Kamati ya Baraza la Vijana la Mkoa
- 4.** Kamati ya Baraza la vijana litaundwa na:
- (a) Mwenyekiti atakayeteuliwa miongoni mwa taasisi za vijana zilizosajiliwa ndani ya Mkoa;
- (b) wajumbe sita watakao wakilisha taasisi za vijana zilizosajiliwa ndani ya mkoa;
- (c) katibu atakayeteuliwa miongoni mwa vijana ndani ya mkoa.
- Makazi
- 5.** Mtu hatakuwa mjumbe wa Baraza la vijana Mkoa na wa Kamati, isipokuwa makazi yake yanatoka Mkoa husika.
- Muda wa kukaa madarakani
- 6.-**(1) Mjumbe yeyote wa Baraza la Mkoa, mbali na mjumbe anayeingia kwa wadhifa wake, kwa kuzingatia masharti ya Jedwali hili, atakaa madarakani kwa muda usiozidi miaka mitatu, kwenye mashauri yatakayoanishwa kwenye hati ya uteuzi ya mjumbe huyo, lakini anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja.
- (2) Uteuzi wa Baraza utafanywa kwa kupitia Tangazo la Serikali.
- Uwazi wa ofisi
- 7.-**(1) Mjumbe wa Baraza la Mkoa, mbali na mjumbe anayeingia kwa wadhifa wake, ataweza-
- (a) katika wakati wowote kuacha kazi katika ofisi kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa Waziri;
- (b) kuondolewa ofisi na Waziri kama mjumbe, iwapo-
- (i) hajahudhuria vikao vitatu mfululizo vya Baraza la Mkoa bila kupewa ruhusa na Mwenyekiti;
- (ii) amepatikana na hatia ya kosa la jinai au amehukumiwa kifungo;

- (iii) ameshindwa kutekeleza majukumu yake kutokana na magonjwa ya kiakili na kimwili kwa muda mrefu au hawezi kutekeleza majukumu yake kama mjumbe wa Baraza la Mkoa; au
- (iv) ameshindwa kufuata masharti ya Sheria hii.

Mikutano ya Baraza

**8.-(1)** Baraza la Mkoa litakutana mara mbili kwa mwaka.

(2) Bila kujali masharti ya aya ndogo (1), Mwenyekiti au wajumbe watatu wengine wa Baraza la Mkoa wanaweza kuitisha mkutano maalum muda wowote pale inapohitajika kwa ajili ya shughuli za Baraza la Mkoa, kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa wajumbe katika siku zisizopungua saba.

(3) Wajumbe wa Baraza la Mkoa katika kikao cha kwanza cha Baraza la Mkoa, watachagua kutoka miongoni mwao Makamu Mwenyekiti.

(4) Isipokuwa robo tatu ya wajumbe wote wa Baraza la Mkoa wanakubali vinginevyo, angalau siku kumi na nne watatoa taarifa ya kila mkutano wa Baraza la Mkoa na kupewa kila mjumbe wa Baraza la Mkoa.

(5) Akidi ya uendeshaji wa shughuli za Baraza la Mkoa itakuwa ni mbili ya tatu ya wajumbe, bila ya Katibu.

(6) Mwenyekiti ataongoza kila kikao cha Baraza la Mkoa ambacho yupo, lakini asipokuwepo, Makamu Mwenyekiti ataongoza, na asipokuwepo, wajumbe waliopo watachagua mmoja kutoka miongoni mwao ambaye kwa ajili ya mkutano huo na shughuli inayofanywa hapo atakuwa na mamlaka yote ya Mwenyekiti.

(7) Isipokuwa kama maamuzi ya pamoja hayatafikiwa, maamuzi yoyote mbele ya Baraza la Mkoa yatakuwa ya wajumbe wengi waliopo na kupiga kura, na pale kura zitakapolingana, Mwenyekiti au mtu anayeongoza kikao hicho atakuwa na kura ya turufu.

(8) Kwa kuzingatia aya ndogo (5), taratibu za uendeshaji wa vikao vya Baraza la Mkoa havitokuwa halali kwa sababu tu ya kuwepo kwa nafasi wazi ya mjumbe katika kikao hicho.

(9) Azimio la maandishi au maazimio yaliyo yenye nyaraka mbalimbali zinazofanana, kila moja likiwa limetiwa saini na wajumbe wa Baraza la Mkoa, litakuwa halali na litatumika kama vile limepitishwa na kikao kilichoitishwa na kupitishwa kihalali.

(10) Kwa kuzingatia masharti ya Jedwali hili, Baraza la Mkoa linaweza kuamua utaratibu wake na utaratibu wa kamati yoyote ya Baraza la Mkoa na kuhudhuria kwa mtu yeyote katika mikutano na linaweza kutengeneza kanuni pamoja na mambo mengine kuhusu-

- (a) mwenendo na usimamizi wa masuala ya Baraza la Mkoa;
- (b) namna ya malipo yote ikijumuisha, hundi, hati fungani na hati nyingine za malipo na stakabadhi zote za fedha zilizolipwa kwenye Baraza la Mkoa, zitasainiwa, kutolewa, kukubaliwa, kupitishwa au vinginevyo kutekelezwa; na
- (c) taratibu za mikutano na shughuli nyingine za Baraza la Mkoa.

Kumbukumbu

**9.** Baraza la Mkoa litasaidia kutayarishwa kwa kumbukumbu za maazimio yote na taarifa za mienendo ya mikutano ya Baraza kuwekwa katika vitabu maalum kwa ajili hiyo.

Lakiri ya  
Baraza la  
Vijana la  
Mkoa

**10.**-(1) Lakiri ya Baraza la Mkoa utahifadhiwa na Katibu au na mtu mwingine kama ambavyo Baraza la Mkoa litakavyoamuru, na hautatumika ila kwa amri ya Baraza la Mkoa.

(2) Lakiri ya Baraza la Mkoa, utakapopigwa katika nyaraka na kuthibitishwa, utakubalika na kutambulika kisheria na isipokuwa vinginevyo ikithibitishwa, amri yoyote au ridhaa ya Baraza la Mkoa chini ya kifungu hiki itachukuliwa kuwa imetolewa hivyo.

(3) Lakiri ya Baraza la Mkoa utathibitishwa kwa kutiwa saini ya Katibu wa Baraza la Mkoa.



**JEDWALI LA TATU**

*(Linatengenezwa chini ya kifungu cha 10(5))*

**UTEUZI, MUDA WA KUKAA MADARAKANI, MIKUTANO NA MASUALA  
MENGINE YA  
UTARATIBU WA BARAZA LA WILAYA**

Muundo wa  
Baraza la  
Vijana la  
Wilaya

1. Baraza la Vijana la Wilaya litaundwa na:
  - (a) Mwenyekiti;
  - (b) Wajumbe wote wa Kamati ya Vijana Wilaya; na
  - (c) Wawakilishi thelathini kutoka taasisi za vijana zilizosajiliwa ndani ya Wilaya.

Jukumu la  
mamlaka ya  
serikali za  
mitaa

2. Mamlaka ya Serikali za mitaa katika eneo la Baraza la Vijana la Wilaya litakuwa na jukumu la uangalizi wa kazi na muundo wa Baraza la Vijana la Wilaya.

Uundwaji wa  
Kamati za  
Vijana za  
Wilaya

- 3.-(1) Baraza la Vijana la Wilaya litaunda Kamati itakayoitwa Kamati ya Vijana ya Wilaya.
- (2) Kamati ya Vijana ya Wilaya itakuwa chombo cha Baraza la Vijana la Wilaya.

Muundo wa  
Kamati ya  
Baraza la  
Vijana la  
Wilaya

4. Kamati la Baraza la vijana litaundwa na:
  - (a) Mwenyekiti atakayeteuliwa miongoni mwa taasisi za vijana zilizosajiliwa ndani ya Wilaya;
  - (b) wajumbe sita watakao wakilisha taasisi za vijana zilizosajiliwa ndani ya Wilaya;
  - (c) katibu atakayeteuliwa miongoni mwa vijana ndani ya Wilaya.
- (2) Endapo taasisi za vijana zilizosajiliwa zitakuwa zaidi ya sita, ujumbe wao utakuwa wa kupokezana.

- Makazi **5.** Mtu hatakuwa mjumbe wa Baraza la Vijana la Wilaya na wa Kamati, isipokuwa makazi yake yanatoka Wilaya husika.
- Muda wa kukaa madarakani **6.**-(1) Mjumbe yeyote wa Baraza la Wilaya, mbali na mjumbe anayeingia kwa wadhifa wake, kwa kuzingatia masharti ya Jedwali hili, atakaa madarakani kwa muda usiozidi miaka mitatu, kwenye mashauri yatakayoanishwa kwenye hati ya uteuzi ya mjumbe huyo, lakini anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja.  
(2) Uteuzi wa Baraza la Wilaya utafanywa kwa kupitia Tangazo la Serikali.
- Uwazi wa ofisi **7.**-(1) Mjumbe wa Baraza la Wilaya, mbali na mjumbe anayeingia kwa wadhifa wake, ataweza-  
(a) katika wakati wowote kuacha kazi katika ofisi kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa Waziri;  
(b) kuondolewa ofisi na Waziri kama mjumbe, iwapo-  
(i) hajahudhuria vikao vitatu mfululizo vya Barazala Wilaya bila kupewa ruhusa na Mwenyekiti;  
(ii) amepatikana na hatia ya kosa la jinai au amehukumiwa kifungo;  
(iii) ameshindwa kutekeleza majukumu yake kutokana na magonjwa ya kiakili na kimwili kwa muda mrefu au hawezi kutekeleza majukumu yake kama mjumbe wa Baraza la Wilaya; au  
(iv) ameshindwa kufuata masharti ya Sheria hii.
- Mikutano ya Baraza **8.**-(1) Baraza la Wilaya litakutana mara tatu kwa mwaka.  
(2) Bila kujali masharti ya aya ndogo (1), Mwenyekiti au wajumbe watatu wengine wa Baraza la Wilaya wanaweza kuitisha mkutano maalum muda wowote pale inapohitajika kwa ajili ya shughuli za Baraza la Wilaya, kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa wajumbe katika siku zisizopungua saba.  
(3) Wajumbe wa Baraza la Wilaya katika kikao cha kwanza cha Baraza la Wilaya, watachagua kutoka miongoni mwao Makamu Mwenyekiti.

(4) Isipokuwa robo tatu ya wajumbe wote wa Baraza la Wilaya wanakubali vinginevyo, angalau siku kumi na nne watatoa taarifa ya kila mkutano wa Baraza la Wilaya na kupewa kila mjumbe wa Baraza la Wilaya.

(5) Akidi ya uendeshaji wa shughuli za Baraza la Wilaya itakuwa ni mbili ya tatu ya wajumbe, bila ya Katibu.

(6) Mwenyekiti ataongoza kila kikao cha Baraza la Wilaya ambacho yupo, lakini asipokuwepo, Makamu Mwenyekiti ataongoza, na asipokuwepo, wajumbe waliopo watachagua mmoja kutoka miongoni mwao ambaye kwa ajili ya mkutano huo na shughuli inayofanywa hapo atakuwa na mamlaka yote ya Mwenyekiti.

(7) Isipokuwa kama maamuzi ya pamoja hayatafikiwa, maamuzi yoyote mbele ya Baraza la Wilaya yatakuwa ya wajumbe wengi waliopo na kupiga kura, na pale kura zitakapolingana, Mwenyekiti au mtu anayeongoza kikao hicho atakuwa na kura ya turufu.

(8) Kwa kuzingatia aya ndogo (5), taratibu za uendeshaji wa vikao vya Baraza la Wilaya havitokuwa batili kwa sababu tu ya kuwepo kwa nafasi wazi ya mjumbe katika kikao hicho.

(9) Azimio la maandishi au maazimio yaliyo yenye nyaraka mbalimbali zinazofanana, kila moja likiwa limetiwa sainsi na wajumbe wa Baraza la Wilaya, litakuwa halali na litatumika kama vile limepitishwa na kikao kilichoitishwa na kupitishwa kihalali.

(10) Kwa kuzingatia masharti ya Jedwali hili, Baraza la Wilaya linaweza kuamua utaratibu wake na utaratibu wa kamati yoyote ya Baraza la Wilaya na kuhudhuria kwa mtu yeyote katika mikutano na linaweza kutengeneza kanuni pamoja na mambo mengine kuhusu-

- (a) mwenendo na usimamizi wa masuala ya Baraza la Wilaya;
- (b) namna ya malipo yote ikijumuisha, hundi, hati fungani na hati nyingine za malipo na stakabadhi zote za fedha zilizolipwa kwenye Baraza la Wilaya, zitasainiwa, kutolewa, kukubaliwa, kupitishwa au vinginevyo kutekelezwa; na
- (c) taratibu za mikutano na shughuli nyingine za Baraza la Wilaya.

Kumbukumbu **9.** Baraza la Wilaya litasaidia kutayarishwa kwa kumbukumbu za maazimio yote na taarifa za mienendo ya mikutano ya Baraza kuwekwa katika vitabu maalum kwa ajili hiyo.

Lakiri ya Baraza la Vijana la Wilaya **10.**-(1) Lakiri ya Baraza la Wilaya utahifadhiwa na Katibu au na mtu mwingine kama ambavyo Baraza la Wilaya litakavyoamuru, na hautatumika ila kwa amri ya Baraza la Wilaya.

(2) Lakiri ya Baraza la Wilaya, utakapopigwa katika nyaraka na kuthibitishwa, utakubalika na kutambulika kisheria na isipokuwa vinginevyo ikithibitishwa, amri yoyote au ridhaa ya Baraza la Wilaya chini ya kifungu hiki itachukuliwa kuwa imetolewa hivyo.

(3) Lakiri ya Baraza la Wilaya utathibitishwa kwa kutiwa saini ya Katibu wa Baraza la Wilaya.

**JEDWALI LA NNE**

*(Linatengenezwa chini ya kifungu cha 11(4))*

**UTEUZI, MUDA WA KUKAA MADARAKANI MIKUTANO NA UTARATIBU MWINGINE WA BARAZA LA KATA**

Muundo wa Baraza la Vijana la Kata **1.** Baraza la Vijana la Kata litaundwa na;  
 (a) Mwenyekiti;  
 (b) Wajumbe wote wa Kamati ya Kata; na  
 (c) Wawakilishi kumi na tano kutoka kwenye vijana wenye sifa ndani ya Kata.

Jukumu la mamlaka ya serikali za mitaa **2.** Mamlaka ya Serikali za mitaa katika eneo la Baraza la Vijana la Kata litakuwa na jukumu la uangalizi wa kazi na muundao wa Baraza la Vijana na Kata.

Uundwaji wa Kamati ya Vijana ya Kata **3.**-(1) Baraza la Vijana la Kata litaunda Kamati itakayoitwa Kamati ya Vijana ya Kata.

(2) Kamati ya Vijana ya Kata itakuwa chombo cha Baraza la Vijana la Kata.

Muundo wa Kamati ya Baraza la Vijana la Kata

4. Kamati ya Baraza la Vijana litaundwa na:
- Mwenyekiti atakayechaguliwa miongoni mwa vijana wenye sifa ndani ya Kata.
  - Wajumbe sita watakaowakilisha vijana kutoka kwenye Kata husika;
  - Katibu atakayeteuliwa miongoni mwa vijana ndani ya Kata.

Makazi

5. Mtu hatakuwa hatakuwa Mjumbe wa Baraza la Vijana la Kata na wa kamati isipokuwa makazi yake yanatoka Kata husika.

**JEDWALI LA TANO**

*(Linatengenezwa chini ya kifungu cha 19(4))*

**UJIRA WA WAJUMBE, MUDA WA KUKAA MADARAKANI, MIKUTANO NA UTARATIBU MWINGINE WA MKUTANO MKUU**

Ujira wa wajumbe wa Mkutano Mkuu

1. Wajumbe wa Mkutano Mkuu watalipwa, katika kuhudhuria mikutano ya Mkutano Mkuu, posho na matumizi mengine kama itakavyoidhinishwa na Waziri.

Muda wa kukaa madarakani

2.-(1) Mjumbe yeyote wa Mkutano Mkuu, mbali na mjumbe anayeingia kwa wadhifa wake, kwa kuzingatia masharti ya Jedwali hili, atakaa madarakani kwa muda usiozidi miaka mitatu, kwenye mashauri yatakayoanishwa kwenye hati ya uteuzi ya mjumbe huyo, lakini anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja.

(2) Wajumbe wa Mkutano Mkuu watateuliwa kwa nyakati tofauti ili muda wao wakumaliza kipindi chao umalizike kwa nyakati tofauti.

(3) Uteuzi wa Mkutano Mkuu utafanywa kwa kupitia Tangazo la Serikali.

Uwazi wa ofisi

**3.-(1)** Mjumbe wa Mkutano Mkuu, mbali na mjumbe anayeingia kwa wadhifa wake, ataweza-

- (a) katika wakati wowote kuacha kazi katika ofisi kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa Waziri;
- (b) kuondolewa ofisi na Waziri kama mjumbe, iwapo-
  - (i) hajahudhuria vikao vitatu mfululizo vya Mkutano Mkuu bila kupewa ruhusa na Mwenyekiti;
  - (ii) amepatikana na hatia ya kosa la jinai au amehukumiwa kifungo;
  - (iii) ameshindwa kutekeleza majukumu yake kutokana na magonjwa ya kiakili na kimwili kwa muda mrefu au hawezi kutekeleza majukumu yake kama mjumbe wa Mkutano Mkuu; au
  - (iv) ameshindwa kufuata masharti ya Sheria hii.

Mikutano ya  
Mkutano  
Mkuu

**4.-(1)** Mkutano Mkuu utakutana mara moja kwa mwaka.

(2) Bila kujali masharti ya aya ndogo (1), Mwenyekiti au wajumbe watatu wengine wa Mkutano Mkuu wanaweza kuitisha mkutano maalum muda wowote pale inapohitajika kwa ajili ya shughuli za Mkutano Mkuu, kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa wajumbe katika siku zisizopungua saba.

(3) Wajumbe wa Mkutano Mkuu katika kikao cha kwanza cha Mkutano Mkuu, watachagua kutoka miongoni mwao Makamu Mwenyekiti.

(4) Isipokuwa robo tatu ya wajumbe wote wa Mkutano Mkuu wanakubali vinginevyo, angalau siku kumi na nne watatoa taarifa ya kila mkutano wa Mkutano Mkuu na kupewa kila mjumbe wa Mkutano Mkuu.

(5) Akidi ya uendeshaji wa shughuli za Mkutano Mkuu itakuwa ni mbili ya tatu ya wajumbe, bila ya Katibu.

(6) Mwenyekiti ataongoza kila kikao cha Mkutano Mkuu ambacho yupo, lakini asipokuwepo, Makamu Mwenyekiti ataongoza, na asipokuwepo, wajumbe waliopo watachagua mmoja kutoka miongoni mwao ambaye kwa ajili ya mkutano huo na shughuli inayofanywa hapo atakuwa na mamlaka yote ya Mwenyekiti.

(7) Isipokuwa kama maamuzi ya pamoja hayatafikiwa, maamuzi yoyote mbele ya Mkutano Mkuu yatakuwa ya wajumbe wengi waliopo na kupiga kura, na pale kura zitakapolingana, Mwenyekiti au mtu anayeongoza kikao hicho atakuwa na kura ya turufu.

(8) Kwa kuzingatia aya ndogo (5), taratibu za uendeshaji wa vikao vya Mkutano Mkuu havitokuwa batili kwa sababu tu ya kuwepo kwa nafasi wazi ya mjumbe katika kikao hicho.

(9) Azimio la maandishi au maazimio yaliyo yenye nyaraka mbalimbali zinazofanana, kila moja likiwa limetiwa sainsi na wajumbe wa Mkutano Mkuu, litakuwa halali na litatumika kama vile limepitishwa na kikao kilichoitishwa na kupitishwa kihalali.

(10) Kwa kuzingatia masharti ya Jedwali hili, Mkutano Mkuu linaweza kuamua utaratibu wake kuhudhuria kwa mtu yeyote katika mikutano na linaweza kutengeneza kanuni pamoja na mambo mengine kuhusu-

- (a) mwenendo na usimamizi wa masuala ya Mkutano Mkuu;
- (b) namna ya malipo yote ikijumuisha, hundi, hati fungani na hati nyingine za malipo na stakabadhi zote za fedha zilizolipwa kwenye Mkutano Mkuu, zitasainiwa, kutolewa, kukubaliwa, kupitishwa au vinginevyo kutekelezwa; na
- (c) taratibu za mikutano na shughuli nyingine za Mkutano Mkuu.

Kumbukumbu

5. Mkutano Mkuu litasaidia kutayarishwa kwa kumbukumbu za maazimio yote na taarifa za mienendo ya mikutano ya Mkutano Mkuu kuwekwa katika vitabu maalum kwa ajili hiyo.

Lakiri ya  
Mkutano  
Mkuu

6.-(1) Lakiri ya Mkutano Mkuu utahifadhiwa na Katibu au na mtu mwingine kama ambavyo Mkutano Mkuu litakavyoamuru, na hautatumika ila kwa amri ya Mkutano Mkuu.

(2) Lakiri ya Mkutano Mkuu, utakapopigwa katika nyaraka na kuthibitishwa, utakubalika na kutambulika kisheria na isipokuwa vinginevyo ikithibitishwa, amri yoyote au ridhaa ya Mkutano Mkuu chini ya kifungu hiki itachukuliwa kuwa imetolewa hivyo.

(3) Lakiri ya Mkutano Mkuu utathibitishwa kwa kutiwa saini ya Katibu wa Mkutano Mkuu.

**JEDWALI LA SITA**

*(limetungwa chini ya kifungu 23(4))*

**MUDA WA KUKAA MADARAKANI, TARATIBU ZA UTEUZI  
NA MASUALA MENGINE YA TARATIBU ZA BODI**

- |                          |   |
|--------------------------|---|
| Muda wa kukaa madarakani | <p><b>1.</b> Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi, kwa kuzingatia masharti ya Jedwali hili, atakaa madarakani kwa muda usiozidi miaka mitatu kwenye masharti yanayoweza kuainishwa katika hati ya uteuzi, lakini anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja.</p>  |
| Taratibu za uteuzi       | <p><b>2.</b> Wajumbe wa Bodi watateuliwa kwa nyakati tofauti ili muda wao wa kumaliza kipindi chao umalizike kwa nyakati tofauti.</p>   |
| Uwazi wa ofisi           | <p><b>3.</b> Mjumbe wa Bodi anaweza-</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>(a) kuacha kazi katika wakati wowote kwa kumuandikia Waziri taarifa ya maandishi ya kuacha kazi;</li> <li>(b) kuondolewa katika ofisi kama ni mjumbe, iwapo-             <ul style="list-style-type: none"> <li>(i) hajaudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi bila kupewa ruhusa na Mwenyekiti;</li> <li>(ii) amepatikana na hatia ya kosa la jinai na amehukumiwa kifungo;</li> <li>(iii) ana matatizo ya kiakili au kimwili kwa muda mrefu;</li> <li>(iv) ameshindwa kutekeleza majukumu yake kama mjumbe wa Bodi.</li> </ul> </li> </ul> |
| Akidi                    | <p><b>4.</b> Akidi ya kikao cha Bodi itakuwa mbili ya tatu ya wajumbe wote.</p>   |
| Azimio la Bodi           | <p><b>5.</b> Azimio la kikao cha Bodi litapitishwa kwa kura nusu ya kura za wajumbe waliokuwepo, isipokuwa Mwenyekiti, ambaye atakuwa na kura ya turufu tu.</p>   |




**Na.12** *Sheria ya Baraza la Vijana la Taifa* **2015** **73**

Kumbukumb  
u

**6.** Bodi itasaidia kumbukumbu za vikao vya Bodi kuwekwa kwenye vitabu maalum kwa ajili hiyo.

Imepitishwa na Bunge tarehe 31 Machi, 2015.



THOMAS D. KASHILILAH  
Katibu wa Bunge